# Wakulima mwani waiangukia serikali upatikanaji wa sok

WAKULIMA wa zao la mwani, Kisiwani Pemba, wameiomba serikali kuingilia kati upatikanaji wa soko la zao hilo.

Wamesema kwa klufanya hivyo kutawasaidia kuwanusuru na hali ngumu ya maisha wanayokabiliana nayo kutokana na wanunuzi kusitisha ununuaji zao hilo.

Hayo yalibainishwa na wanakikundi cha Muungano kilichopo Shehia ya Makangale, Wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba, alipozungumza na Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alipowatembelea ili kukagua maendeleo ya kikudi hicho.

Haji Hamad Haji ambaye ni miongoni mwa wanakikundi, alisema licha ya wananchi wengi Zanzibar kuhamasika kuzalisha kwa wingi zao hilo, lakini kukosekana kwa soko kunazidi kudumaza hali zao.

"Ukija vijijini watu tunateseka sana na zao hili, migongo imevunjika kwa kuzalisha mwani lakini manufaa hakuna, sasa hivi tumevuna tumebaki kuuweka ndani kutokana na kukosa wa kumuuzia," alisema

Aliongeza kuwa changamoto hiyo inatokana na wananchi kukosa taaluma zaidi ya namna ya kusarifu mwani kwa matumizi mengine, jambo ambalo linasababisha wengi kutegemea njia moja ya uuzaji bila kuwa na mbadala wake.

Naye, Mwenyekiti wa kikundi hicho, Time Ismail Ali, alisema tangu wanunuzi wasitishe kununua zao hilo ambalo kwa kiwango kikubwa linazalishwa na wanawake, limesababisha familia nyingi kukumbwa na hali ngumu ya maisha.

"Kusema ukweli soko la mwani limetuathiri sana wakulima hapa Makangale hususan wanawake kwa kuwa wengi hiki ndicho kilimo chetu. Tulikuwa tukipata angalau fedha kidogo ya kujikimu na familia zetu, lakini hali imekuwa tofauti tangu kampuni zisitishe kununua mwani. Tunavuna sana lakini upo ndani unaoza hatuna pa kupeleka," alisema.

Kutokana na hilo, aliiomba serikali kusaidia kumaliza changamoto hiyo ili hali iendelee kwa kuwa hivyo inahatarisha kutokea madhara zaidi kwa wananchi wanaotegemea zao hilo.

"Tunaiomba serikali kama ilivyofanya katika karafuu basi ituangalie na wakulima wa mwani kwa kuwa hali ni mbaya kwa sasa, tunatumia nguvu nyingi kuzalisha, lakini ikifika wakati wa kuuza wateja hakuna kama ambavyo ili sasa na hata mteja akipatikana bei ya bado ni ndogo ikilinganishwa na gharan za uzalishaji," alisema.

Awali, Mkurugenzi wa TAMWA Zanzib Dk. Mzuri aliwataka wakulima hao kutoka tamaa na uzalishaji ili kujiendeleza kichu licha ya changamoto zinazowakabili.

"Kikubwa tuendelee na uzalisha tusirudi nyuma kwa kuwa ndiyo shughu zetu. Wadau tutajitahidi kuwasilish changamoto zenu sehemu husik ili zitafutiwe ufumbuzi na kilimo hik kiwakomboe kama mazao mengine yanayolimwa hapa Zanzibar," alisema.

**Changamoto**

**UUZAJI**

Wakulima wa mwani wanalalamika kwamba ukosefu wa soko la uhakika la zao hilo, unawasababishia kukata tamaa katika kilimo.

Uhuru Uk.10, July 1, 2021

Scanned with CamScanner

